## Hoja za Kisheria Unazopaswa Kufahamu

- **Kusomewa mashtaka:** Kikao cha mahakama ambapo mshtakiwa huelezwa rasmi mashtaka na kuweka ombi la: kutopinga mashtaka (hapingi ukweli), kukiri mashtaka (kukubali mashtaka) au kukataa kukiri (kukataa mashtaka).
- **Dhamana: Kiasi cha pesa ambacho mshtakiwa anapaswa kulipa ili kutoka gerezani kutokana na mashtaka.**
- **Kudumu au Kuendelea:** Kucheleweshwa kwa kikao cha mahakama hadi siku nyingine.
- **Mshtakiwa:** Mtu anayeshtumiwa.
- **Kikao cha mahakama:** Taratibu ya mahakama wakati jaji anasikiliza maelezo ili kutoa uamuzi.
- **Mlalamishi:** Katika kesi ya kihalifu, hatua ya serikali ya kuleta mashtaka dhidi ya mshtakiwa.
- **Kikao cha kabla ya hukumu:** Tarehe ya kikao cha mahakama ambapo kiongozi wa mashtaka na mwanasheria wa upande wa utetezi hukutana ili kujadili dhana za kweli za kesi.
- **Kiongozi wa mashtaka:** Wakili wa serikali anayewakilisha kesi dhidi ya mshtakiwa.
- **Hukumu:** Kikao cha mahakama ambapo jaji huamua kuhusu adhabu kwa mshtakiwa.
- **Hati ya kuitwa mahakamani:** Hati ya kisheria inayomwamrisha shahidi kuonekana mahakamani.
- **Ushahidi:** Taarifa za shahidi, aliyeapishwa, katika mahakama.
- **Uamuzi:** Kikao cha mahakama cha kuamua matokeo ya kesi baada ya kuwasilishwa kwa ushahidi na ushuhuda wa shahidi.



Ili upate maelezo zaidi kuhusu kuweka mpango wa usalama, nyenzo za jamii au mipango na huduma za dhuluma za kinyumbani katika eneo lako, wasiliana na mpango wa dhuluma za kinyumbani ulio karibu nawe:

Ohio Domestic Violence Network ODVN

**Mtandao wa Dhuluma za Kinyumbani wa Ohio:**
**800-934-9840 au 614-781-9651**
**www.odvn.org**

Ili upate maelezo kuhusu usaidizi wa kisheria wa bila malipo tafadhali wasiliana na Huduma za Kisheria za Ohio:
**866-lawohio (866-529-6446)**
**www.ohiolegalhelp.org**

Ohio Domestic Violence Network ODVN

The Ohio Domestic Violence Network (ODVN is a statewide coalition of domestic violence programs, supportive agencies, and concerned individuals working together to stop domestic violence through education, information and training for those who are affected by domestic violence, and by promoting social and systems change.

This project is supported by Grant No. G-1901OHSDVC awarded by the Department of Health & Human Services, Administration for Children and Families (ACF), Administration on Children, Youth, and Families (ACYF), Family and Youth Services Bureau (FYSB). The opinions, findings, conclusions, and recommendations expressed in this publication, program, exhibition are those of the author and do not necessarily reflect the views of the Department of Health & Human Services.

**SWAHILI CRIMINAL COURTS BROCHURE**

# DHULUMA ZA KINYUMBANI NI UHALIFU



Ohio Domestic Violence Network ODVN

Dhuluma za kinyumbani ni mtindo wa udhibiti wa kimabavu. Baadhi ya vitendo vya dhuluma za kinyumbani ni uhalifu Ohio. Unaweza kupiga simu kwa vyombo vya utekelezaji wa sheria au uende kwa ofisi ya kiongozi wa mashtaka wa eneo lako ili uripoti uhalifu.

**Hatari huongezeka mara nyingi pindi unapoanza kufikiria kuhusu na kuchukua hatua za kujitenga au kutamatisha uhusiano na mtu anayekunyanyasa.** Huenda chaguo za kisheria zikatoa kiwango fulani cha ulinzi lakini hazikuhakikishii usalama. Ni muhimu kuwa na mpango wa usalama unapotumia mfumo wa kisheria wa kihalifu au kiraia. Wasiliana na mpango wa dhuluma za kinyumbani wa eneo lako ili upate maelezo zaidi kuhusu kuweka mpango wa usalama.

## Hatua katika Kesi la Kosa Dogo

Tafadhali kumbuka kuwa hatua hizi ni za kawaida, lakini huenda kesi yako ikawa tofauti. Ili upate maelezo zaidi mahususi kuhusu kesi mahususi ya kihalifu, tafadhali wasiliana na wakili wa eneo lako au ofisi ya kiongozi wako wa mashtaka.

1. Uhalifu huripotiwa na mwathiriwa, shahidi au vyombo vya kutekeleza sheria.
2. Vyombo vya kutekeleza sheria au kiongozi wa mashtaka huamua kuwa kuna ushahidi wa kutosha wa kuwasilisha mashtaka.
3. Mhalifu hukamatwa au samansi (ilani ya kuonekana mahakamani) hutolewa kwa mshtakiwa. Hili linaweza kutokea katika eneo la tukio la uhalifu au baadaye.
4. Wakati wa (au wakati mwingine kabla ya) kushtakiwa, mshtakiwa husikiliza mashtaka, anaweza kuomba kupata mwanasheria na kuweka ombi. Dhamana hutayarishwa. Mwathiriwa anaweza kuomba Amri ya Ulinzi ya Muda Mfupi (TPO). Iwapo ombi litakuwa la kutokiri mashtaka, basi kikao kingine cha mahakama (kikao cha kabla ya hukumu) huwekwa.
   a. **Wakati mwingine, mshtakiwa huachiliwa kwa dhamana bila ya kikao cha mahakama au kabla ya kikao cha mahakama kuratibiwa. Hii inaweza kumaanisha kuwa huna fursa ya kuomba TPO kabla ya kuachiliwa kwa mshtakiwa. Iwapo una wasiwasi wa wakati huo kuhusu usalama, wasiliana na wakili au mwanasheria wa eneo lako mara moja. Usingoje hadi kufanyika kwa mashtaka ndipo uzungumzie mahitaji yako ya usalama.**
5. Iwapo ombi litakuwa la kutokiri mashtaka, mijadala inaweza kuwasilishwa na/au makubaliano ya ombi yanaweza kuafikiwa wakati wa kikao cha kabla ya hukumu au wakati wowote kabla ya hukumu kuanza. Iwapo ombi litakuwa la kukiri au la kutopinga mashtaka, mahakama inaweza kuenda mara moja katika awamu ya kutoa hukumu (angalia hatua ya 8).
6. Iwapo hamna makubaliano ya ombi yatakayoafikiwa, hukumu hutendeka katika idadi ya siku zilizowekwa, isipokuwa mshtakiwa asalimishe haki zake ili kuharakisha hatua ya kutoa hukumu.
7. Jaji au jopo la majaji wa mahakama humpata mshtakiwa na hatia au la.
8. Iwapo atapatikana na hatia, huenda jaji akatoa hukumu au kuweka tarehe ya kutoa hukumu. Mwathiriwa ana haki ya kutoa taarifa kuhusu jinsi uhalifu umeathiri maisha yake kabla ya jaji kuamua kutoa hukumu.
9. Hukumu (adhabu) inaweza kujumuisha: kifungo cha gerezani, udhibiti wa jamii, kulipa fidia na/au kulipa faini. Udhibiti wa jamii ni muundo wa ufuatiliaji (unaofanywa na ofisa wa urekebishaji wa tabia au ukaguzi wa kompyuta tu) ili kuhakikisha kuwa mshtakiwa anafuata sheria ambazo jaji anatoa. Masharti ya urekebishaji wa tabia zinaweza kujumuisha: kukaa mbali na mtu au eneo, kutovunja sheria, kukamilisha huduma kwa jamii, kuenda kupata ushauri, kukamilisha matibabu ya dawa za kulevya au pombe, kuhudhuria mafunzo ya kukinga kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu au kitu chochote au kulipa fidia (kulipa pesa kwa mwathiriwa kwa gharama zinazohusiana na uhalifu).
   a. **Matokeo haya yanayoweza kutokea huenda yakawa au yasiwe ya usaidizi kwako kupata au kuwa salama. Iwapo una maswali kuhusu usalama wako na jinsi hukumu inavyoweza kuathiri hali yako, tafadhali wasiliana na wakili.**

Hatua katika kosa la jinai ya dhuluma za kinyumbani ni tofauti; zungumza na wakili wako au ofisi ya kiongozi wa mashtaka ya eneo lako ili upate maelezo zaidi iwapo mshtakiwa atahukumiwa kwa kosa la jinai.

## Ni nini maana ya Amri ya Ulinzi ya Muda Mfupi (TPO)?

Baada ya uhalifu kutendeka na wakati wowote katika kipindi cha kesi ya uhalifu, mwathiriwa anaweza kuomba kupata TPO kupitia kwa mahakama ya uhalifu. Hii ni amri ya muda mfupi ambayo inatumika hadi kukamilika kwa kesi ya uhalifu ili kupiga marufu vitendo vya mtu aliyeshtakiwa (Mshtakiwa) kama vile:

- Kuwasiliana na mwathiriwa kwa njia ya simu, barua ya posta, Barua pepe au kupitia kwa mtu mwingine.
- Kumkaribia mwathiriwa, bila kujali eneo.
- Kuishi katika makazi yanayoshirikiwa na mwathiriwa.
- Kuzuia matumizi ya huduma.

Wakati mwingine TPO inaweza kujumuisha watoto. Kwa kawaida TPO huombwa wakati wa kusomewa mashtaka, lakini huenda usiwe na fursa ya kuomba TPO kabla ya kuachiliwa kwa mshtakiwa iwapo alikamatwa. Ni muhimu pia kukumbuka kuwa TPO hukamilika wakati kesi ya uhalifu inapokamilika, hali ambayo inaweza kutokea katika tarehe yoyote ya kikao cha mahakama au katikati ya tarehe za vikao vya mahakama bila wewe kujua.

**Ukiukaji wa Amri ya Ulinzi ya Muda Mfupi ni hatia.** Iwapo mshtakiwa atakiuka TPO, piga simu kwa vyombo vya kutekeleza sheria au ofisi ya kiongozi wa mashtaka ya eneo lako mara moja. Ili kujadili chaguo zako za usalama, wasiliana na wakili au mwanasheria wa eneo lako haraka iwezekanavyo.

## Fahamu Haki Zako!

Kama mwathiriwa, una haki ya:

- Kushughulikiwa kwa haki na heshima kwa usalama, hadhi na faragha yako;
- Baada ya kutuma ombi, kupata ilani ya taratibu zote za umma na kuhudhuria;
- Kusikilizwa katika vikao vingi vya mahakama kuhusu kesi;
- Kupata ulinzi unaofaa dhidi ya Mshtakiwa au mtu yeyote anayemwakilisha;
- Baada ya kutuma ombi, kupata ilani inayofaa ya hatua yoyote ya kuachiliwa au kutoroka kwa Mshtakiwa;
- Kukataa kuhojiwa, kuhamishwa au ombi lolote la ugunduzi lililofanywa na au kwa niaba ya Mshtakiwa;
- Kulipwa fidia (kufidiwa kwa hasara ya kibiashara) kutoka kwa Mshtakiwa;
- Kupata taratibu zisizo na ucheleweshaji usiofaa na ukamilishaji wa kesi kwa wakati;
- Baada ya kutuma ombi, kuzungumza na kiongozi wa mashtaka; na
- Kufahamishwa, kwa maandishi kuhusu haki zako zote
- Kuandamana na wakili wa mwathiriwa katika kila taratibu za mahakama.
- Kuomba kupata Amri ya Ulinzi ya Muda Mfupi (TPO) katika kesi hii
- Kutotishiwa au kushurutishwa na mtu ili usiweze kutoa ushahidi. Iwapo mtu yeyote– mtu anayekunyanyasa, mwanasheria wa mtu anayekunyanyasa au mtu mwingine– anasema au kufanya kitu chochote ili kukufanya uogope kushirikiana katika kesi, mweleze wakili wako na kiongozi wa mashtaka mara moja.

Baadhi ya haki hizi zinahitaji uziombe ili kuzipata. Ili upate usaidizi kupata haki zako katika maandishi, tembelea **www.ocvjc.org/marsys-law** na "Upate Fomu."

Ohio Domestic Violence Network
ODVN

**odvn.org | 800-934-9840**